

Kongamano la Wadau wa Sekta Binafsi

MAUDHUI YA SHERIA NA KANUNI KUHUSU USHIRIKISHWAJI WA WANANCHI: JUKUMU LA EWURA KATIKA USHIRIKISHWAJI WA WATANZANIA

na

Mha. Charles S. Omujuni
MKURUGENZI WA GESI ASILIA

Dar es Salaam, 23rd Februari 2018

YALIYOMO

1. Utangulizi
2. Sheria ya Petroli, 2015
3. Kanuni za Ushirikishwaji wa Watanzania, 2017
4. Majukumu ya EWURA katika Mpango wa Ushirikishwaji wa Watanzania
5. Hitimisho

UTANGULIZI

UTANGULIZI (1)

- "Ushirikishwaji wa Wananchi" kwa Tanzania maana yake ni nini? Ni falsafa ya kuhakikisha kuwa siku zote tuhakikishe wawekezaji wa nje-

  (a) wanatumia huduma za ndani za viwango;
  (b) wananunua bidhaa za ndani za viwango;
  (c) wanaajiri wananchi kwa idadi kubwa;
  (d) wanaingia ubia (kwa hisa) na wananchi;
  (e) wanachangia kuhamishia teknolojia nchini.

- Falsafa ya "Ushirikishwaji wa Wananchi" siku zote HAIPENDWI na wawekezaji wa kutoka nje, hivyo inapingwa sana na makampuni makubwa duniani kwa kutumia vigezo mbalimbali.

UTANGULIZI (2)

- "Ushirikishwaji wa Wananchi" katika miradi mikubwa ya kuvuna rasilimali za asili (kama gesi asilia) si falsafa ngeni kwa mujibu wa Azimio la Umoja wa Mataifa Na. 1802 la 14 Desemba1962.
- Kanuni ya Chimbuko (Rule of Origin) ni sehemu ya Mikataba ya Biashara Huru (Free Trade Agreements (FTA)), ambapo thamani ya bidhaa (Value Content) ni kigezo muhimu na cha msingi.
- Nchi za Mashariki ya Mbali (China, Korea na Japan), Asia (Singapore, Indonesia na Malaysia), Amerika ya Kusini (Chile, Peru,T&T

UTANGULIZI (3)

- Katika bara la Afrika, nchi za Ghana, Nigeria, Sierra Leone, Afrika Kusini, Uganda, Kenya, Botswana, Msumbiji na Tanzania tayari zimeonesha umuhimu wa kushirikisha wananchi katika miradi ya madini, mafuta na gesi asilia.
- Nchi zilizotekeleza falsafa ya "Ushirikishwaji wa Wananchi" duniani tangu mwaka 1920 hadi sasa zilifanikiwa sana. Baadhi ya nchi hizo ni Norway, Japan, China, Korea, Singapore, Malaysia, Chile, Brazil, Peru, Afrika Kusini, Ghana na Nigeria.
- Nchi nyingi zilitunga Sheria ili kuipatia nguvu za kisheria falsafa ya "Ushirikishwaji wa Wananchi"

UTANGULIZI (4)

- Sheria ya Petroli, 2015 inalipatia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania ("TPDC") wajibu wa kushamirisha "Ushirikishwaji wa Watanzania" katika shughuli za petroli (mafuta na gesi asilia).
- Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli ("PURA") na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji ("EWURA") husimamia utekelezaji wa falsafa hii kupitia kwa wenye leseni na wakandarasi wao.
- Wizara ya Nishati ("MoE"), Baraza la Uwezeshaji la Taifa ("NEEC") na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania ("TPSF") huandaa

UTANGULIZI (5)

- Katika mada hii, sikusudii kuongelea kiundani wajibu wa TPDC" wala "PURA", "NEEC" au "TPSF". Isipokuwa baadhi yake nitazitaja katika kuwaandaa Watanzania washiriki katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi ("EACOP").
- Kwa kuwa majukumu ya EWURA ni kwenye Mkondo wa Kati na wa Chini ("Midstream and Downstream") wa Tasnia ya Petroli (mafuta na gesi asilia), nitajielekeza kwenye "EACOP".
- Chini ya Umoja wa Wafanyabiashara Duniani ("WTO"), wakubwa wa umoja huo wanapinga kwa nguvu kubwa utekelezaji wa falsafa ya "Ushirikishwaji wa Wananchi".

UTANGULIZI (6)

- Kupitia WTO (GATT, TRIMS, GATS, na ASCM) wanaziba uwezekano, kwani wanapinga-

  (a) matumizi ya neno "wananchi" ("national treatment") ambalo huhimiza upendeleo wa wazawa dhidi ya wawekezaji wa kigeni; na

  (b) kuweka viwango vya kufikiwa ("qualitative restrictions") ni kushamirisha ubaguzi.

- Falsafa ya "Ushirikishwaji wa Wananchi" ikitekelezwa katika nchi zinazoendelea, ikiwemo Tanzania, mataifa makubwa yanatikisika sana pasipo SABABU ZA MSINGI. Sisi sote tunaihitaji FALSAFA HII SASA, hivyo

SHERIA YA PETROLI, 2015

SHERIA YA PETROLI (1)

- Hivi karibuni, hapa Tanzania, Bunge la Jamhuri ya Muungano, lilitunga Sheria ya Petroli, 2015.
- Ni Sheria mpya inayoainisha udhibiti wa mikondo mitatu ya petroli; inaanzisha Kampuni ya Mafuta ya Taifa (NOC), na Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA).
- Sheria inatambua na kuainisha majukumu ya EWURA, PURA, na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC, ambayo ndiyo NOC).
- Sheria imeipatia TPDC jukumu la kushamirisha Ushirikishwaji wa Watanzania, wakati PURA na EWURA ni wadhibiti wa mipango hiyo.

SHERIA YA PETROLI (2)

- Kifungu cha 219(1) – Bidhaa na huduma za ndani (kwa mfano, huduma za ujenzi, malazi, sheria, bima, na benki) sharti zitolewe na Watanzania au Kampuni za Ndani.
- Kifungu cha 219(2) - Pale ambapo bidhaa au huduma muhimu zitakosekana nchini, bidhaa au huduma hizo, sharti zitolewe na Kampuni ya nje yenye ubia (JV) na Kampuni za Ndani.
- Kifungu cha 219(3) - Kampuni ya Ndani inayotajwa kwenye kifungu 219(2) sharti ishiriki kupata hisa zisizopungua 25% katika ubia au kiwango kingine kilichowekwa kwenye KANUNI.

SHERIA YA PETROLI (3)

- Kifungu cha 219(4) - Wenye kupewa leseni, wakandarasi, na wasaidizi wao watatakiwa kutayarisha Mipango wa Manunuzi wa Miaka 5 na kuiwasilisha PURA, ikibainisha mahitaji.
- Kifungu cha 219(5) – Atakayepewa leseni, wakandarasi, na wasaidizi wao watatakiwa kuijulisha PURA kuhusu mahitaji ya ubora wa viwango, mikataba inayotarajiwa, na utekelezaji wa Mpango wa Ushirikishwaji wa Watanzania.
- Kifungu cha 219(6) – Waliotajwa kwenye Kifungu cha 219(1) sharti wawe na uwezo wa kuongeza thamani kwa Viwango vya Mazingira.

SHERIA YA PETROLI (4)

- Kifungu cha 219(7) – Ndani ya siku 60 baada ya mwisho wa mwaka, wenye leseni watawasilisha Taarifa ya Mafanikio ya Utekelezaji wa Mpango wa Ushirikishwaji wa Watanzania kwa PURA.
- Kifungu cha 219(8) – Wote wenye leseni watawasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango kwa mujibu wa KANUNI, na Programu ya Kuendeleza Watoa Huduma, iliyopitishwa.
- Kifungu cha 219(9) – Kampuni ya Ndani kwa mujibu wa Sheria ya Kampuni, ni Kampuni inayomilikiwa 100% na Watanzania au Kampuni yenye ubia na Watanzania au

SHERIA YA PETROLI (5)

- Kifungu cha 220(1) – Ndani ya mwaka mmoja baada ya wenye leseni na wakandarasi watawasilisha Programu ya Ajira na Mafunzo kwa mwaka unaofuata ili ipitishwe na PURA.
- Kifungu cha 220(2) – Programu ya Ajira na Mafunzo kwa Watanzania sharti iwe kwa kipindi chote cha Mradi na izingatie jinsia, usawa, ulemavu, jamii ya wenyeji, na kupokeza vyeo kwa mujibu wa Sheria ya Ajira ("Sura ya 366").
- Kifungu cha 220(3) – Endapo PURA itakuwa imepitisha Programu ya Mafunzo ya Kulipiwa na Mwekezaji ("Sponsorships"), isibadilishwe bila kupata kibali cha PURA.

SHERIA YA PETROLI (6)

- Kifungu cha 220(5) – Jamii ya wenyeji ("Host Community") ni wakazi halisi wa eneo ambalo shughuli za mafuta na gesi zinaendelea.
- Kifungu cha 221 – Huweka msisitizo kuhusu umuhimu wa kuhamishia Mafunzo na Teknolojia mpya kwa Watanzania.
- Kifungu cha 222 – Huweka msisitizo kuhusu Wajibu wa Mwekezaji kwa Jamii ("Corporate Social Responsibility (CSR)") kupitia Serikali za Mitaa.
- Kifungu cha 223 – Huweka msisitizo kwenye umuhimu wa Kiapo cha Uadilifu, ambacho kila mwekezaji itabidi akiingie mwanzoni na kukiishi.



KANUNI ZA USHIRIKISHWAJI WA WATANZANIA

KANUNI ZA USHIRIKISHWAJI (1)

- Waziri wa Wizara ya Nishati, kwa mujibu wa Kifungu cha 258(2)(b)(xv) alitunga Kanuni za Ushikishwaji wa Watanzania na kuzitangaza tarehe 5 Mei 2017.
- Kanuni za Ushirikishwaji wa Watanzania zilianza kutumika nchini Tanzania tarehe 5 Novemba 2017 (miezi sita baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali).
- Lengo sahihi la Kanuni za Ushirikishwaji wa Watanzania ni kutoa ufafanuzi kuhusu masuala mahsusi yaliyoainishwa kwenye Sheria ya Petroli, 2015. Wawekezaji katika Tasnia ya Petroli walihusishwa sana hadi mwisho.

KANUNI ZA USHIRIKISHWAJI (2)

- Kanuni ya 4 - Ushirikishwaji wa Watanzania unayo malengo yafuatayo-
  - (a) kushamirisha Ongezeko la Thamani na Ajira kwa kutumia wataalam, bidhaa, huduma, biashara, na fedha za ndani;
  - (b) kuendeleza uwezo wa ndani katika tasnia ya petroli kupitia elimu, kuhamisha ujuzi na programu za utafiti;
  - (c) kupunguza sana tatizo la kutokuajiriwa kwa kutumia bidhaa na huduma katika shughuli za petroli;
  - (d) kuongeza ubora wa uwezo wa ndani na ushindani wa kimataifa katika biashara;

KANUNI ZA USHIRIKISHWAJI (3)

(e) kuanzisha visaidizi vya Tasnia ya Petroli vitakavyosaidia kudumisha maendeleo ya kiuchumi;

(f) kuanzisha na kudumisha kabisa usimamizi wa Mipango ya Maendeleo kwa kutumia Watanzania; na

(g) kuweka utaratibu wa wazi na imara wa kupima mafanikio ya utekelezaji na kupata Taarifa za Ushirikishwaji wa Watanzania.

- Kanuni ya 5 – Inaweka misingi mitatu (3) ya Ushirikishwaji wa Watanzania katika Shughuli za Petroli (mafuta na gesi asilia), ambayo ni-

KANUNI ZA USHIRIKISHWAJI (4)

(a) huduma kwa wenye leseni, wakandarasi na wasaidizi wao zitapatikana kwa upendeleo maalum, kwanza kabisa, kuhakikisha watoa huduma wa ndani wanapata kazi na bidhaa zinazozalishwa nchini zinauzwa, endapo zitakidhi viwango vya ubora vya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) au vya kimataifa.

(b) Watanzania wenye sifa za kuajiriwa, elimu na ujuzi wapewe kipaumbele cha kwanza cha kuajiriwa; na

(c) Mafunzo kazini kwa Watanzania yapewe kipaumbele na umuhimu kwa kipindi chote cha Mradi wa Petroli.

KANUNI ZA USHIRIKISHWAJI (5)

- Kanuni ya 6 – Mawasiliano ya Sera, taratibu na wajibu wa Ushirikishwaji wa Watanzania ni kwa wenye leseni, wakandarasi na wasaidizi wao.
- Kanuni ya 8 – Ushirikishwaji ni kutoa kipaumbele cha kwanza kuajiri Watanzania wenye sifa, kununua bidhaa na huduma za ndani, na kuhamishia nchini teknolojia baada ya utafiti.
- Kanuni ya 9 – Inawataka wenye leseni, wakandarasi, na wasaidizi wao kutayarisha na kuwasilisha Mpango Kamilifu wa Ushirikishwaji wa Watanzania kwa Mamlaka husika (PURA au EWURA) ili ipitishwe.

KANUNI ZA USHIRIKISHWAJI (6)

- Kanuni ya 10 – Inaweka taratibu za Mamlaka husika (PURA au EWURA) na muda wa kudurusu na kupitisha au kutopitisha Mpango ya Ushirikishwaji wa Watanzania.
- Kanuni ya 11 – Inaainisha yaliyomo kwenye Mpango wa Ushirikishwaji wa Watanzania.
- Kanuni ya 12 – Inafafanua masuala ya ajira kwenye shughuli za petroli.
- Kanuni ya 13 – Inasisitiza umuhimu wa kuandaa Mpango wa Kupokezana Vyeo ("Succession Plan") kwenye shughuli za petroli.

KANUNI ZA USHIRIKISHWAJI (7)

- Kanuni ya 13 – Inafafanua maana ya ajira zisizohitaji ujuzi na zenye kuhitaji ujuzi wa kati. Hapa, INASISITIZWA kuwa, kwa vyovyote vile, ajira hizo hazitaruhusiwa kutoka nje ya Tanzania.
- Kanuni za 15 hadi 28 – Zinatoa ufafanuzi wa malengo ya taifa kwenye manunuzi, utafiti, uhamishaji wa teknolojia, huduma za bima, za kisheria, za uhandisi, na za kifedha.
- Kanuni ya 31- Inaweka utaratibu wa wenye leseni, wakandarasi na wasaidizi wao kuwasilisha Mpango wa Manunuzi ili upitishwe na Mamlaka husika (PURA au EWURA).

KANUNI ZA USHIRIKISHWAJI (8)

- Kanuni za 36 na 37 – Zinazipatia Mamlaka husika (PURA au EWURA) kuandaa Mfumo wa Sifa Hitajika za Pamoja ("Common Qualification System").
- Kanuni ya 38 – Zinazitaka Mamlaka husika (PURA au EWURA) kuandaa, kutunza, kuhuisha na kila mwaka kutangaza Kanzidata ("website") ya Watanzania wenye uwezo wa kuuza bidhaa na kutoa huduma ("LSSP") kwenye shughuli za petroli, ambapo ndipo PEKEE, wakandarasi na wasaidizi wao watanunua huduma za viwango.

- Kanuni za 43 hadi 48 – Zinazungumzia mambo

WAJIBU WA EWURA KATIKA KUTEKELEZA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI

WAJIBU WA EWURA KATIKA USHIRIKISHWAJI (1)

- Wajibu wa EWURA katika Ushirikishwaji wa Watanzania umeainishwa kwenye Sheria ya Petroli, 2015 na Kanuni za Ushrikishwaji wa Watanzania, 2017.
- Kwa kuwa EWURA ni mdhibiti wa Mikondo ya Kati na Chini wa Petroli (uchakataji wa mafuta na gesi ghafi, usafirishaji, usambazaji na uuzaji wa mafuta na gesi asilia) inashughulika na Ushirikishwaji wa Watanzania katika Mikondo hiyo.
- Wajibu wa KWANZA ni kuweka mazingira na Kanzidata ya utekelezaji na usimamizi wa falsafa ya Ushirikishwaji wa Watanzania.

WAJIBU WA EWURA KATIKA USHIRIKISHWAJI (2)

- Kanuni ya 4(2)(a) – Inaitaka EWURA kutayarisha Kanzidata (“Baseline Data”) ya kutambua uwezo wa ndani wa wauzaji bidhaa na watoa huduma kwenye Tasnia ya Petroli (mafuta na gesi asilia) ili waajiriwe.
- Kanuni ya 4(2)(b) – Inataka EWURA kuainisha mahitaji (“Needs Assessment”) ya ndani ya kuajiri Watanzania wenye sifa.
- Kanuni ya 4(2)(c) – Inaitaka EWURA kuainisha maeneo yenye mapungufu ya uwezo wa kushiriki (“area with no capacity or capabilities”) kwenye Tasnia ya Petroli nchini Tanzania.

WAJIBU WA EWURA KATIKA USHIRIKISHWAJI (3)

- Kanuni ya 4(3)(a) – Inaitaka EWURA, kwa kushirikiana na asasi nyingine, kuanzisha Mfumo wa Ushirikishwaji wa Watanzania katika kuhamishia teknolojia nchini Tanzania.
- Kanuni ya 4(3)(b) – Inaitaka EWURA, kwa kushirikiana na asasi nyingine, kuweka mikakati ya kufuatilia utekelezaji wa falsafa ya Ushirikishwaji wa Watanzania nchini.
- Kanuni ya 10(1) – Inaitaka EWURA, ndani ya siku 28 baada ya kupokea Mpango wa Ushirikishwaji wa Watanzania, kutoa matokeo baada ya kudurusu Mpango huo.

WAJIBU WA EWURA KATIKA USHIRIKISHWAJI (4)

- Kanuni ya 12 – Inaitaka EWURA kupokea na kudurusu Taarifa ya Nusu Mwaka ya Ajira kutoka kwa wenye leseni na wakandarasi kuhusu Ushirikishwaji wa Watanzania.
- Kanuni ya 15(4) na (5) – Inataka EWURA kupitisha mapendekezo ya mabadiliko ya Kampuni ya Ubia kushirikisha Watanzania.
- Kanuni ya 19 – Inaitaka EWURA kupendekeza Serikalini (Wizara ya Fedha kupitia Wizara ya Nishati) mazingira mazuri kwa Watanzania kupata ya vivutio vya kifedha kwa watakaowekeza kuhamishia teknolojia nchini.

WAJIBU WA EWURA KATIKA USHIRIKISHWAJI (6)

- Kanuni ya 30 – Inaitaka EWURA kusimamia kuwa mchakato wa manunuzi hauathiri Ushirikishwaji wa Watanzania.
- Kanuni ya 31 – Inaitaka ndani ya siku tisini (90) baada ya kuanza shughuli za petroli, EWURA kupokea na kudurusu Mpango wa Manunuzi.
- Kanuni ya 32 – Inaitaka EWURA, kutafakari Taarifa ya wakandarasi watakayowasilisha baada ya kufanya manunuzi ya dharura.
- Kanuni za 36 na 37 – Zinaitaka EWURA kuandaa Mfumo wa Sifa Hitajika za Pamoja ("CQS") ili utumike kuchuja wenye ujuzi.

WAJIBU WA EWURA KATIKA USHIRIKISHWAJI (7)

- Kifungu cha 126(3)(c) cha Sheria ya Petroli – EWURA ihakikishe kuwa NOC ikiomba kibali cha kujenga miundombinu ya petroli iwe imewasilisha Mpango wa Ushirikishwaji wa Watanzania.
- Kifungu cha 132(c) cha Sheria ya Petroli – Kabla EWURA haijatoa leseni ya shughuli za petroli kwa Mkondo wa Kati, sharti mwombaji wa leseni awasilishe Mpango wa Ushirikishwaji wa Watanzania.
- Kifungu cha 143(1)(c) cha Sheria ya Petroli – EWURA itafuta leseni endapo mwenye leseni akikosa mfululizo kutimiza mahitaji ya Mpango.

WAJIBU WA EWURA KATIKA USHIRIKISHWAJI (8)

- Katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi ("EACOP") kutoka Hoima (nchini Uganda) hadi Tanga (nchini Tanzania), EWURA ni mdhibiti wa njia hii ya kusafirisha mafuta.
- Hivi karibuni (mwaka 2018), EACOP itawasilisha maombi ya leseni ya kusafirisha mafuta ghafi kupitia nchini Tanzania, EWURA itapokea maombi hayo, itayachakata, na kutoa leseni.
- Kwa kuwa, asilimia 80 ya bomba (km 1,147) zitajengwa na kudumu nchini Tanzania, Sheria ya Petroli na Kanuni zake zitatumika kudhibiti shughuli za ufundi, uchumi na usalama za

WAJIBU WA EWURA KATIKA USHIRIKISHWAJI (9)

- EWURA inashiriki katika Timu ya Majadiliano ya ya Serikali kuhusu Mkataba ("Host Government Agreement") na viambatisho vyake.
- EWURA inakusanya Taarifa za Watanzania na kujenga Kanzidata ("website") ya Watanzania wenye Uwezo wa Kuuza Bidhaa na Kutoa Huduma ("LSSP") kwenye Shughuli za Petroli.
- EWURA inashirikiana na Baraza la Uwezeshaji Tanzania ("NEEC"), Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania ("TPSF"), ITV na hata Mamlaka ya Udhibiti wa Petroli ya Uganda ("PAU") kutoa elimu kwa umma na kuwaandaa ili washiriki

HITIMISHO

HITIMISHO (1)

- Tukubaliane kwa pamoja, kuwa falsafa ya Ushirikishwaji wa Watanzania katika Miradi yote mikubwa ya Shughuli za Petroli ni bora na yenye manufaa kwetu sote.
- Kila mmoja wetu anayo kazi ya kufanya ili kubadili sura ya sasa (ya unyonge), kuwa na sura mpya ya matumaini kuwa Watanzania wanaweza.
- Ninawaombeni Watanzania tujitokeze kwa wingi, tujisajili kwenye Kanzidata ya LSSP, kwani ukiachwa tarehe 28 Feb 2018, tutakuwa tumeshindwa sisi. Wakandarasi watachagua majina yaliyomo kwenye Kanzidata.

HITIMISHO (2)

- Fursa ziko lukuki kuanzia kwenye ajira, kuuza bidhaa, kutoa huduma, kushiriki kuwekeza, kushiriki kuhamishia teknolojia na tafiti nchini.
- Endapo unataka kushiriki kwa kuajiriwa, wasiliana na TAESA (Ofisi ya Waziri Mkuu) au kupitia tovuti ya NEEC (www.uwezeshaji.go.tz) jisajili, wao watashughulikia maombi yako.
- Tafadhali ingia kwenye tovuti www.ewura.go.tz kujisajili EWURA ili wawekezaji rasmi wachague miongoni mwao hao watakaosajiliwa.
- Tuongozwe na kauli kuwa “Inawezekana

NEVER
GIVE UP
ON
YOUR
DREAMS